



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA



ZABUNI YA UWAKALA WA UENDESHAJI WA RADIO ULANGA FM  
(ZABUNI NA. LGA/082/2022/2023/NC/06)


Tarehe: 11/01/2023

**Kwa: WAZABUNI WOTE**

1. Mwaliko huu wa Zabuni (MZ) unafuatia Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga kwa mwaka wa fedha 2022/2023 lililotangazwa katika mbao za matangazo.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imetenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya kumpata Wakala wa Uendeshaji wa Radio Ulanga FM na inakusudia kutumia sehemu ya fedha hiyo kwa ajili ya malipo ya mwendeshaji wa Radio atakayepatikana na kuingia Mkataba wa uendeshaji wa Radio Ulanga FM.
3. Hivyo, kwa tangazo hili Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga inaalika Makampuni, Ushirika, Taasisi, Vikundi vya watu Vilivyosajiliwa Kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu kuwasilisha maombi ya Zabuni zao kwa ajili ya Uendeshaji wa Radio Ulanga FM kama ilivyoainishwa kwenye *Kabrasha la Zabuni*.
4. Zabuni hii inafanyika kwa njia ya Zabuni ya Kitaifa kamailivyoainishwa kwenye Kanuni za Manunuzi ya Umma Na. 446 za mwaka 2013 na ipo wazi kwa Wazabuni wote kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni.
5. Kabrasha la Zabuni husika linapatikana kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, S.L.P 22, Mahenge.



6. Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga kabla ya tarehe **25/01/2023 saa 5:00 asubuhi**. Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilishwa Zabuni.
7. Wazabuni wote ambao watakuwa na nia ya kuomba Zabuni husika wanaweza kupata maelezo ya ziada kuhusiana na Nyaraka / Zabuni husika katika Ofisi ya Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi kuanzia saa 1:30 – 9:30 siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko ya Kitaifa.
8. Kabrasha la Zabuni husika linapatikana kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, S.L.P 22, Mahenge / Ulanga.
9. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa katika muundo usiokubalika hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini, bila kujali mazingira yoyote.

  
Saida Mahugu

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
ULANGA

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
ULANGA